# Programu ya Huduma za Afya Ngazi ya Jamii (CBHP)

# YALIYOMO

- Historia ya huduma za afya ngazi ya jamii
- Programu ya Kitaifa ya Huduma za Afya Ngazi ya Jamii
- Mazingira rafiki kwa Programu.

# Historia ya Huduma za Afya Ngazi ya Jamii

## Baada ya uhuru,

Serikali ilidhamiria kuboresha huduma za afya kwa

- Kuanzisha Shule za madaktari na wauguzi
- Ila ikadhihirika kwamba
  - Huduma za afya za mijini zilionekana kuboreshwa zaidi na zilitumia gharama kubwa
  - Huduma za vijijini ziliendelea kuzorota kwa kukosa ubora na hazikuwafikia wengi

# Historia ya Huduma za Afya Ngazi ya Jamii

## Miaka ya 60 hadi 70

- Magonjwa na vifo maeneo ya vijijini yaliendelea kuongezeka
- Sehemu zilizokuwa na huduma za afya ya jamii haikuzitumia kutokana na mila potofu
- Vyanzo vya magonjwa na vifo vilidhibitiwa kwa kiasi kikubwa katika ngazi ya jamii na pale iliposhindikana basi wagonjwa walipelekwa kituo cha afya
- Uzoefu wa Tanzania ulipelekea nchi mbalimbali kuanzisha huduma za afya ya msingi na kutumia wahudumu wa afya katika ngazi ya jamii

# Historia ya Huduma za Afya Ngazi ya Jamii

## Miaka ya 70 hadi 80:

Katika miaka hiyo Azimio la afya ya msingi lilitolewa na lilisema kwamba:

- Huduma za afya ni haki ya kila mtu anapohitaji
- Huduma za afya ya msingi ziwe za kujitosheleza na zitolewa kwa usawa
- Huduma za kinga zilipewa kipaumbele kuliko zile za tiba
- Wahudumu wa afya ngazi ya jamii watumike kutoa huduma za afya katika jamii mfano lishe, chanjo huduma za uzazi na mtoto.

## Miaka ya 80 na kuendelea:

- Wafadhili hawakupendelea huduma hizi hivyo walianzisha huduma za msonge na kuzifadhili mfano: Programu ya Malaria,UKIMWI,Kifua Kikuu na Ukoma.n.k

# Hali ya sasa ya Huduma za Afya Ngazi ya Jamii

- Huduma nyingi za msonge zinafadhiliwa na wadau wa maendeleo
- Watoa huduma waliopo wanajitolea, na sio rahisi kuwawajibisha pale wanapokosea
- Ni za muda mfupi na sio endelevu
- Hazipo kwenye mipango kazi ya halmashauri
- Zinalenga zaidi magonjwa kama HIV, TB na hali nyingine za afya mfano lishe na afya ya uzazi wa mama na mtoto
- Mafunzo yanatofautiana, muda, mada na hata malipo na vitendea kazi

# Mpango wa Taifa wa Huduma za Afya Ngazi ya Jamii

Serikali imedhamiria kurudisha huduma za afya ngazi ya jamii kama zilivyokuwa zamani kwa:

- Kuboresha uratibu ngazi zote
- Kuunganisha miradi misonge na kutoa huduma kwa pamoja kwa kutumia mtoa huduma wa afya ngazi ya jamii
- Kuunganisha huduma za afya ngazi ya jamii na zile za vituo vya afya
- Kutoa mafunzo yenye viwango vya ubora
- Kuajiri kada ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii

# Yaliyokwisha fanyika mpaka sasa

- Kuandaa mwongozo wa kisera (2014) na Mpango Mkakati (2014 – 2020) wa huduma za afya ngazi ya jamii unaoelekeza wahudumu wa afya
  - Wachaguliwe na vijiji vyenyewe
  - Wapatiwe mafunzo ya ngazi ya cheti na tayari mtaala umekwisha andaliwa na mafunzo yameshaanza kutolewa katika vyuo vilivyofanyiwa tathmini.
  - Waajiriwe na kupatiwa mishahara na mafao ya uzeeni
  - Watoe huduma jumuishi za kuzuia na kudhibiti magonjwa yote pia kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa afya bora

# Inaendelea……………

- Waratibu wa CBHP Mikoa yote wameshapatiwa mafunzo **elekezi (RCBHPco orientations meeting)** juu ya utekelezaji wa programu ya CHW katika Mikoa husika
- Uteuzi wa waratibu wa CBHP ngazi ya Wilaya umeshatekelezwa kwa H/W zote saba
- Maelekezo kuhakikisha elimu ya afya kwa Jamii inatolewa kila siku katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya yameshatolewa
- Miongozo mbali mbali ya Health promotions kama sera,mipango mikakati ya taifa imeshapelekwa katika H/W zote saba

# Karibuni kwa majadiliano
# ASANTENI!!